MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIANO NA 24.

KWA NEEMA MMEOKOLEWA

Soma: Warumi 5

NEEMA

Katika Biblia neema ya Mungu maana yake wema wa kupenda watu Haistahili kabisa kwa mwanaume au mwanamke yeyote na ni karama ya hiari ya Mungu. Zaidi imeeleweka wazi katika zawadi ya Mungu kwa Bwana Yesu kufikiliza wokovu Utahitajika kukumbuka hili wazi kama ukijifunza somo hili

Jambo Ia uhai na mauti

Sisi sote tunajuwa vema mno tu kwamba uhai wetu utaisha karibu au baadaye mauti yanapotujia Mungu alimtuma Mwanawe, Bwana Yesu Kristo ulimwenguni ili kuifungua njia ya uzima. Njia hii ya wokovu kutoka mautu ni kiini cha Injili ya Kikristo.

Dhambi zetu zimetutenga na Mungu, ambaye ni asili ya uzima wote. Yesu alikuja ili amlete mwanadamu kwa Muumba, kwa kuionyesha njia ya uzima. Mtu anaweza kuijua Biblia yake kwa ukamilifu toka Mwanzo hadi Ufunuo; anaweza kufahamu vema mafundisho ya Biblia-lakini hiyo hataokoka kwa hilo. Hawezi kuwa na tumaini la uzima, ha akubali dhabihu ambayo Yesu ameifanya kwa ajili yake katika unyenyekevu wa kweli.

Namna ya kufikiri vibaya

Watu wengi wanadhani kwamba mambo mema wanyo yafanya na mabaya wanayotenda ni nyongeza ya kuona jinsi wanavyo simama mbele za Mungu. Wanafikiri kuwa, kwa mda yanapo kuwepo mema zaidi kuliko ubaya, wana ***haki*** kwenye upendo wa Mungu. Hii tu Sio kweli!

26B (a) Andika toka Mathayo 25:31-32.
(b) Ni nani “Mwana wa Adamu” katika mstari wa 31?
(c) Watazawadiwa nini wenye haki kama unavyo sema mstariwa 34?
(d) Wenye haki wamefanya kitu gani ambacho wenye kutenda maovu wasio haki ambacho hawakufanya?

26C Watu gani hawata hukumiwa?

27A Andika orodha ya mambo mema baadhi ambayo Mungu ameahidi kwa wale ambao watapewa sehemu kwenye Ufalme wake.

27B Tafuta kile Biblia inachosema kuhusu watakatifu. Tazama mistari hii ya fungu la maneno halafu andika maelezo mafupi ya kila mmoja unachosema:
1. Matendo 9:13,22
2. Matendo 26:10
3. Warumi 8:27
4. Warumi 16:2,15
5. Waefeso 3:8

Tuma majibu yako kwa:

Jina lako ni:

Christadelphian Bible Mission Box CBM, 404 Shaftmoor Lane,
Birmingham B28 8SZ, England

MASWALI KARATASI YA 7

Jaribu na njibu maswali katika maneno yako mwenyewe, Kwenye “kazi ya ziada” unaweza kujibu au kuacha kama utaona ni magumu sana. Tafadhali jibu maswali jibu maswali yote mengine.

MASOMO 24-27

24A Eleza jinsi tunavyo weza kuokolewa.

24B Sema kwa maneno yako kwa “neema” ina maana gani.

24C Kazi ya ziada
Ina maana gani “Tuendelee katika dhambi ili neema izidi” (Warumi 6)

25A Ipi ni njia sahihi ya kueleza mwamini wa kweli ambaye amekufa?
Ame: (a) pita; (b) amekwenda mbinguni; (c) amelala.

25B (a) Toa sababu za kuonyesha kwamba Yesu hakuwa roho wakati alipo fufuka toka wafu.
(b) Kazi ya ziada: Unaweza kutoa fungu la maneno jingine lolote mbali ya Luka 24 ili kusaidia jibu lako kwa swali (a)?
(c) Je, waamini watakuwa na miili wakati watakapo toka kwa wafu.
(d) Kazi ya ziada: Unaweza kutoa kutoka katika Biblia mstari ili kusaidia jibu la sehemu (c)?

25C (a) Katika Yohana 11, Mariamu alisema nini mara alipo muona Yesu?
(b) Lazaro alitokaje nje ya kaburi?
(c) Yohana 12:10-11 inatuambia nini kuhusu makuhani wakuu?

25D Kazi ya ziada
Mstari upi katika Yohana 5 unao sema kwamba:
(a) Mungu ameweka hukumu zote kwa Mwanawe.
(b) Wakati una kuja ambao wote walio makaburini watasikia sauti ya Yesu.
(c) Kama tukisikia maneno ya Yesu na kumwamini basi tutaweza kupita toka mautini kwenda uzimani.

26A Weka matukio haya katika mpangilio sahihi:
UFUFUO / KURUDI KWA YESU / KUUSIMAMISHA UFALME / HUKUMU

Hata wengi wanao dai kuwa ni Wakristo na wanakiri kwamba Mungu amelipa gharama kubwa ya kuleta wokovu, wanaona inawabidi kupata baraka hii ya mambo wanayo yafanya.

Ni rahisi mno kwetu sisi kufikiri inatubidi ***tupate*** zawadi za Mungu. Lakini zawadi haiwezi kupatikana. ***Mshahara*** tu ndio unapatikana, na Paulo anatuambia:

> *"Mshahara wa dhambi ni mauti; bali zawadi ya Mungu ni uzima katika Yesu Kristo Bwana wetu" (Warumi 6:23).*

Ni rahisi sana kwa sisi kuangukia katika namna hi mbaya ya kufikiri. Mungu amefanya mengi kwa ajili yetu, tunataka kuonyesha shukrani zetu kwa kumpendeza Yeye: na hivyo tunakuja kufikiri kwamba mambo tunayo yafanya "yamelipwa" kwa baraka za Mungu.

Ni moja ya mafundisho ya Maandiko muhimu zaidi ambapo msamaha wa dhambi na uzima wa milele katika Ufalme wa Mungu ni zawadi **za** Mungu, nazo hazipatikani au kulipia.

Mafundisho ya Maandiko yasemaje

- sisi sote ni wenye dhambi tumehukumiwa mauti
- hatuwezi kujiokowa wenyewe, na inatubidi tuwe na unyenyekevu kukubali hili;
- Mungu ametoa njia ya wokovu katika Bwana Yesu Kristo
- njia hii ipo wazi kama tuna imani (au kusadiki) Injili, inayopatikana katika Neno la Mungu, Biblia.

Kumwamini Mungu

Somo kwa makini maneno haya:

"Mungu, aliye mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu, alitupenda sisi, hata wakati tulikuwa wafu katika dhambi) alituhuisha pamoja na Kristo (kwa neema mmeokolewa); na ametufufua pamoja naye, na kutufanya kuketi pamoja naye katika Sehemu za mbinguni katika Kristo Yesu; ili katika zamani zijazo aonyeshe wingi wa neema yake upitao kiasi kwa wema wake kwetu sisi katika Kristo Yesu. Maana kwa neema mmeokolewa, kwa njia ya imani: ambayo haikutokana na nafsi zenu ni kipawa cha Mungu; wa/a Si kwa matendo mtu asije akajisifu." (Waefeso 2:4-9)	Upendo wa Mungu kwetu ni tele, hata kama tuwenye dhambi, na ametufanya kuwa hai pamoja na Kristo. (Wokovu huu ni zawadi.) Ametupa hii sehemu ya juu katika Yesu, kwa hivyo wakati ujao atatubariki sisi zaidi (pamoja na uzima katika Ufalme Wake). Wokovu huu ni kipawa cha Mungu. Tuna hitaji kumwamini Yeye. Hatuwezi **kufanya** chochote ili kupata wokovu, hivyo hakuna anaye weza kujisifu.

Sasa soma Warumi 3:20-28 kwa makini sana. Utaona kwamba ujumbe ni uleule. Hakuna ambacho Wayahudi wanaweza kufanya kwa kushika sheria, na hakuna tunachoweza kufanya sisi katika maisha yetu, kuweza kutufanya tuonekane machoni pa Mungu wenye haki. Sote sisi ni wenye dhambi.

Lakini kwa neema yake, Mungu anawahesabia haki wale wanao mwamini Yesu.

26B (a) Andika toka Mathayo 25:31-32.
(e) Ni nani "Mwana wa Adamu" katika mstari wa 31?
(f) Watazawadiwa nini wenye haki kama unavyo sema mstariwa 34?
(g) Wenye haki wamefanya kitu gani ambacho wenye kutenda maovu wasio haki ambacho hawakufanya?

26C Watu gani hawata hukumiwa?

27A Andika orodha ya mambo mema baadhi ambayo Mungu ameahidi kwa wale ambao watapewa sehemu kwenye Ufalme wake.

27B Tafuta kile Biblia inachosema kuhusu watakatifu. Tazama mistari hii ya fungu la maneno halafu andika maelezo mafupi ya kila mmoja unachosema:
6. Matendo 9:13,22
7. Matendo 26:10
8. Warumi 8:27
9. Warumi 16:2,15
10. Waefeso 3:8

Tuma majibu yako kwa:

Jina lako ni:

Christadelphian Bible Mission Box CBM, 404 Shaftmoor Lane,
Birmingham B28 8SZ, England

MASWALI KARATASI YA 7

Jaribu na njibu maswali katika maneno yako mwenyewe, Kwenye “kazi ya ziada” unaweza kujibu au kuacha kama utaona ni magumu sana. Tafadhali jibu maswali jibu maswali yote mengine.

MASOMO 24-27

24A Eleza jinsi tunavyo weza kuokolewa.

24B Sema kwa maneno yako kwa “neema” ina maana gani.

24C Kazi ya ziada
Ina maana gani “Tuendelee katika dhambi ili neema izidi” (Warumi 6)

25A Ipi ni njia sahihi ya kueleza mwamini wa kweli ambaye amekufa?
Ame: (a) pita; (b) amekwenda mbinguni; (c) amelala.

25B (a) Toa sababu za kuonyesha kwamba Yesu hakuwa roho wakati alipo fufuka toka wafu.
(e) Kazi ya ziada: Unaweza kutoa fungu la maneno jingine lolote mbali ya Luka 24 ili kusaidia jibu lako kwa swali (a)?
(f) Je, waamini watakuwa na miili wakati watakapo toka kwa wafu.
(g) Kazi ya ziada: Unaweza kutoa kutoka katika Biblia mstari ili kusaidia jibu la sehemu (c)?

25C (a) Katika Yohana 11, Mariamu alisema nini mara alipo muona Yesu?
(d) Lazaro alitokaje nje ya kaburi?
(e) Yohana 12:10-11 inatuambia nini kuhusu makuhani wakuu?

25D Kazi ya ziada
Mstari upi katika Yohana 5 unao sema kwamba:
(d) Mungu ameweka hukumu zote kwa Mwanawe.
(e) Wakati una kuja ambao wote walio makaburini watasikia sauti ya Yesu.
(f) Kama tukisikia maneno ya Yesu na kumwamini basi tutaweza kupita toka mautini kwenda uzimani.

26A Weka matukio haya katika mpangilio sahihi:
UFUFUO / KURUDI KWA YESU / KUUSIMAMISHA UFALME / HUKUMU

Mungu na Yesu tu ndio wenye haki, lakini kama tukiamini kuwa Yesu alikufa kwa ajili yetu, na kuikubali dhabihu aliyo tufanyia, Mungu atatusamehe dhambi zetu na kutuhesabia haki. Angalia tena mtume anarudia kuusema ukweli ulio wa muhimu kwamba yote ni ya Mungu, na hakuna mtu awezaye kujisifu kuhusu kuwa ameokoka.

> *"Kwasababu hii, tukisha kuhesabiwa haki itokanayo na imani, tuna amani na Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo: Ambaye kwa yeye pia tumepata njia ya kuingia kwa imani katika neema hii ambayo ndani yake tunasimama, na kufurahi katika tumaini Ia utukufu wa Mungu" (Warumi 5:1-2).*

Mistari hii inatuambia wazi wazi kuhusu nafasi ya mfuasi wa kweli wa Bwana Yesu Kristo Mtu kama huyu ana amani na Mungu, kwasababu ameletwa katika upatano na Mungu kwa njia ya sadaka ya Yesu. Amekubalika na Mungu, na ni mwenyeji wa kipindi kijacho cha Ufalme wa Mungu.

Ameletwa katika urafiki huu kwa kumwamini Mungu. Kwa sababu ya mambo haya, ana njia ya kuingia kwa Mungu - anaweza kumkaribia katika sala. Mwanafunzi kama huyu ameingia kwenye neema.

Je haidhuru tunayo tenda?

Basi, tumeona jinsi mtu anavyoweza kumsogelea Mungu, na kukubalika kwa njia ya neema yake. Mtu kama huyu "amesimama sawa na Mungu".

Lakini hatujasema chochote kuhusu namna mtu anavyotakiwa aishi. Tupo huru, hapo, kujipendeza wenyewe, na kwenda njia zetu wenyewe? Mtume Paulo alifikiri watu wata fikiri namna hiyo. Tayari umesoma sura ya 5 waraka kwa Warumi. Sasa tazama mstari wa kwanza wa sura ya 6, ambayo Inasema:

> *"TuendeIee katika dhambi, ili neema iwe nyingi?"*

Anajibu swali kweli katika mstari unaofuata:

> *"Mungu anakataza. Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?”*

Endelea kusoma hadi mstari wa 14, na uangalie hasa mistari 11 na 12:

> *"Vivyo hivyo nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi kweli, bali walio hai kwa Mungu katika Yesu Kristo Bwana wetu. Kwa sababu hiyo dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti hata mkazitii tamaa zake."*

Kama kweli tunamwamini Bwana Yesu Kristo, tuta **tenda** kama Ikiwa tunamwamini. Tutajaribu vizuri sana kufanya anayo sema. Ndipo tutakuwa wafuasi wake wa kweli.

Kwa upande mwingine, mtu asiye jaribu kufanya mapenzi ya Mungu na kumtii sio mfuasi wa kweli. Kama kweli aliamini, angetii. Hana imani ya kweli, na hivyo hana njia ya kuingia kwenye neema ya Mungu.

Mtume Yakobo anatuambia: "Imani isiyo na matendo, imekufa" (Yakobo 2:17). Imani isiyo mfanya mtu ajitahidi kufuata namna ya maisha ya Kikristo, na kuishinda dhambi ndani yake mwenyewe, Sio imani kabisa.

Maisha mapya katika Kristo

Jinsi gani tunaweza kuonyesha tendo letu Ia kukubali yale Mungu alio tutendea sisi, na kukusudia kwetu kuishi kufuatana na maagizo Yake? Tayari tumesoma Warumi 6, na mstari 1 na 2. Tazama mistari miwili inayofuata:

"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tulio batizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? kwa sababu hiyo tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake: kusudi kama Kristo alivyo fufuka kutoka wafu kwa utukufu wa Baba, hivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."

Yesu alikufa na alifufuka kwa ajili yetu. Nasi tunaungana na sadaka yake, kwa kuzikwa, sio kaburini kama yeye bali katika maji. Huu ni ubatizo wa Kikristo. Wakati mtu anapotoka ndani ya maji, amekuwa "mtu mpya katika Kristo", na yupo tayari kuishi maisha mapya. Amekuwa mfuasi wa kweli wa Bwana Yesu. Wakati huo anaweza kuelezwa kuwa "yumo ndani ya Kristo".

Uzima wa milele sio tu kwa miaka 1000; ni wa milele na milele. Labda hii ni ngumu kwa sisi kufahamu, lakini ni tofauti na maisha ya leo. Wengine wamejaribu kufikiri kwamba uzima wa milele utakuwa ni wa kuchosha. Lakini Mungu asingeweza kamwe kuahidi kitu fulani ambacho kisingekuwa cha kutopendeza.

> *"Maana tangu mwanzo wa ulimwengu, watu hawajasikia, wala kufahamu kwa masikio, wala jicho halikuona Mungu, zaidi yako, aliye mtayarishia yeye amngojae" (Isaya 64:4).*

Hatuwezi kufahamu maajabu ya wakati huo. Wakati shughuli kubwa ya kuwazawadia ya utawala wa Yesu muda wa miaka 1000 ukiisha, kutakuwa na kipindi kizuri zaidi! Kwa maana wakati huo "Mungu atakuwa yote katika wote" (1 Wakorintho 95:28). na kutakuwa na uhusiano kamili kati ya Muumba na viumbe Vyake. Hivi ndivyo Mungu aliplani tangu mwanzo.

Hii ni ahadi ya uzima wa milele.

Muhutasari

1 . Mungu, Yesu na malaika ndio walio na uzima wa kutokufa sasa.
2. Baada ya hukumu, wenye haki (au watakatifu) watapewa uzima wa milele na watafanywa wasife.
3. Watakao fanywa kutokufa watakuwa na miili ya roho. Hawata ona maumivu na hawata weza kufanya dhambi. Watakuwa na nguvu tele za Mungu.

Mafungu ya kusoma: Danieli 12:1-3; Yohana 17; 1 Wakorintho 15:50-57
Jifunze kwa moyo: Yohana 3:16

> *"Maana Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila amwaminie asipotee, bali awe na uzima wa milele."*

*'Tazameni mikono na miguu yangu, kuwa ni mimi: nishike na muone; maana roho haina **mwili na mifupa** kama mnavyo niona mimi" (Luka 24:39).*

Ni wazi kwamba Yesu, akiwa na uzima wa milele, bado alikuwa na mwili na mifupa. Rekodi haituambii kwamba alikuwa na mwili na damu, kwa sababu katika maneno ya Biblia "uhai wa mwili umo katika damu" (Mambo ya Walawi 17:1 1). Kwa maneno mwengine, uhai wa kawaida nguvu zake zimo kwenye damu, lakini sasa Yesu ana ishi kwa uwezo wa Mungu. Wakati Yesu atakapo wapa uzima wa milele watu, miili yao ya kibinadamu itakuja kuwa 'miili ya roho" (1 Wakorintho 15:44,53). Miili yao mipya itatiwa nguvu kwa Roho wa Mungu badala ya damu inayo kufa. Uchungu hautakuwepo, huzuni wala kudhoofika akili au mwili. Kuteseka kwa aina yoyote hakutakuwepo.

“Mungu atayafuta machozi yote toka kwenye macho yao; hakutakuwa na mauti tena, wala huzuni. wala kulia, kamwe hakuta huwa na maumivu tena: maana mambo ya kwanza yamekwisha kupita" (Ufunuo 21:4).

Maajabu ya uzima usio na mwisho!

Njia gani ya ajabu ya kuishi; kuwa na uwezo wa kufurahia mambo mazuri tele anayo tupa Mungu.

Kutakuwa na baraka
- za uzima wa mwili;
- za uwezo wa mwili;
- za chakula kizuri;
- za amani na usalama;
- za kujuwa zaidi yanayo husu mambo ya Mungu.

Hakuta kuwa na kazi ngumu ya kushindana na dhambi kwa kutaka kutenda mema (haki).

Utakumbuka kwamba kwa kitambo kidogo katika karne ya kwanza mitume walipewa zawadi za Roho Mtakatifu. Wengine walihubiri katika lugha mpya; wengine waliponya wagonjwa na kuponya magonjwa ya akili. Hawa walikuwa ni "malimbuko" - wa kuonyesha mavuno ya zawadi kama hizi ambazo watakatifu wa Ufalme wa Mungu watamiliki.

Kuona gani kwa ajabu katika kupita tuliko pewa kwa yajayo!

Ufuasi

Ubatizo ni mwanzo mpya, na dhambi zetu zote za wakati ulio pita zimesamehewa wakati tukibatizwa. Bado, ingawa vigumu tunajaribu, bado tunaendelea kufanya mabaya na kuwaza mambo mabaya.

Lakini kumbuka - Mkristo aliye batizwa anaweza kumjia Mungu kwa njia ya kristo. Anaweza kukiri kushindwa kwake, na kusikitika kwa udhaifu huo. Na Mungu atamsamehe kwa ajili ya Kristo.

Kwa hiyo inatubidi kamwe tusishindwe. Pamoja na upendo wa Baba wa kutusaida sisi, mwisho tutafika kwenye Ufalme wa Mungu, maana, kama Yesu alivyo sema, *"amekusudia Baba kwa mapenzi yake kuwapa Ufalme" (Luka 12:32).*

Umuhimu wa imani

IMANI ni kusadiki au kumwamini Mungu

Mwandishi kwa Waebrania anatuambia kwamba *"pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu"* (Waebrania 11:6). Kuwa na imani ni kumwamini Mungu kabisa, kuweka maisha yetu katika mikono Yake na kumtegemea katika nila zote za maisha yetu, kama mtoto mdogo anavyo mtegemea baba yake, na kumtazama yeye.

Tukiwa na imani ya aina hii, basi kama tulivyo ona, tuna njia ya kuingia kwenye neema ya Mungu. Lakini hatuwezi kuamini kitu chochote kama hatukijui; na hatuwezi kuamini Neno la Mungu, ila tuelewe mafundisho yake.

Ndiyo maana, katika masomo yote ya kozi hii, mafundisho ya Biblia yametiliwa mkazo. Soma wewe mwenyewe Warumi 10:13-17, na uone hasa mstari wa mwisho:

"Hivyo basi imani huja kwa kusikia, na kusikia kwa **neno Ia Mungu.**"

Wafuasi kwenye nyakati za Agano Ia Kale

Ikiwa kusadiki kazi ya Yesu ni muhimu kwa wokovu wetu, patatokea nini kwa watumishi wa Mungu katika nyakati za Agano la Kale? Wataokolewaje, kama waliishi kabla ya Yesu kuja?

Wale walio ishi kwenye Agano la Kale nyakati zile **walijuwa kuhusu Kristo! Hawakumjuwa** kwa jina la Yesu, bali walimjuwa kama mwana wa Mungu aliye ahidiwa - Masihi na Mwana Kondoo wa Mungu.

Walifahamu toka kwenye neno Ia Mungu kuwa watu wote wanahitaji wokovu. Waliambiwa kwamba Mungu atautoa katika kifo cha mtu mkamilifu, ambaye atakuwa ni "Mwana Kondoo wa Mungu", na kutoa uhai wake uhai wake kwa ajili ya wokovu wa watu wote.

Abrahamu alikuwa mmoja wapo kati ya watu wakuu wa Agano la Kale. Wagalatia 3:8 inatuambia kwamba "injili ilihubiriwa kwa Abrahamu", nasi tunasoma jinsi Yesu alivyowa ambia Wayahudi:

> *"Baba yenu Abrahamu alifurahi kuiona siku yangu: aliiona naye alifurahi" (Yohana 8:56).*

Hivyo Abrahamu na wengi wengineo wa Agano la Kale walimwamini Kristo, kama sisi, ingawa walikuwa hawana nafasi kubwa kama sisi, ya kuweza kusoma masimulizi ya Injili ambayo yanatuambia sisi kuhusu maisha na kazi ya Yesu.

Sababu Agano Ia Kale na Jipya, yanatuambia habari ya neema ya Mungu kwenye kazi ya wokovu wetu, tunatakiwa kusoma Biblia yote, na sio Agano Jipya pekee yake tu.

Muhutasari

Hakuna mtu anayeweza kujiokowa mwenyewe - na hakuna anaye weza kuokolewa pasipo unyenyekevu.
Ni neema ya Mungu ndio inayo leta wokovu: neema hii inatuleta kwenye habari njeme za kazi ya Yesu na Ufalme wa Mungu.
Inatupasa tuwe na imani ili tufaidike na neema ya Mungu.

Katika masomo 25 na 26 tumezungumzia kufufua wafu na hukumu itakayo fuata wakati Yesu atakapo toa maneno yake. Wale ambao kwa uaminifu wamemfuata Yesu watakuwa ni wale walio itwa "watakatifu" - walio teuliwa kutawala pamoja na Kristo Mfalme kwa kipindi cha miaka 1,000 toka Yerusalemu.

Wanaume na wanawake hawa watapokea uzima wa milele, sio tu kwa sababu utakuwa ni neema ya Mungu kwa uaminifu wao katika kipindi hiki, bali pia kwa sababu itakuwa ni lazima kuwa na mwili mkamilifu na wenye afya ili kutawala katika Ufalme wa Mungu.

Kwa nini hivyo? Katika wakati wetu taratibu za serikali (au kutawala), watawala na wenye amri za serikali mara chache ni wenye haki na wakweli; hawana busara ya kutosha kutatua matatizo ya ulimwengu: mara kwa mara hawana mali au mamlaka ya kufanya mambo mazuri wanayopenda kufanya; na kati yao walio bora, wakati wanapata **kufanya** ili watengeneze baadhi ya maendeleo, wanazeeka au wana ugua na kufa.

Wale walio na uzima wa milele hawata badilika au kudhoofika, na kwa sababu wamechaguliwa na Mungu wata kuwa na busara na haki.

MTAKATIFU NI MWAMINI WA KWELI

"Mtakatifu" maana yake "wekwa kando". Waamini wa kweli sio kama watu wa ulimwengu; wanajaribu kuwawacha Mungu.

Watakatifu wasio kufa watafananaje?

Wengi wanastaajabu kwa jinsi gani watakatifu watafananaje watakapo fanywa kutokufa. Je, watatambulika? Watakula na kulala? Ingawa hatujui mambo yote madogo madogo, Biblia inatupa baadhi ya habari juu ya jambo hili.

Tunajuwa kwamba Abrahamu, lsaka, Yakobo na manabii wote watatambuliwa katika Ufalme (angalia Luka 13:28).

Tuna mfano wa Yesu mwenyewe, wakati alipo tambuliwa kwa uwazi na wanawake fulani na mitume baada ya kufufuka kwake. Alishiriki chakula pamoja na wafuasi. Mwili wake ulikuwa na alama za mateso ya kikatili msalabani. na wanafunzi waliruhusiwa kumgusa.

Ni kweli kwamba kulikuwa na wakati walipostaajabu kama alikuwa ni aina ya roho wakati alipowatokea kwa muujiza mbele yao. Lakini aliwaambia:

Uzima wa milele sio ni kwa kila mtu

Kama kila mmoja kwa kujiendea mwenyewe atapata uzima wa milele hakuta kuwa na maana ya kujitahidi kutii maagizo ya Mungu. Ahadi ya kuishi milele imefanywa tu kwa wale ambao wanatafuta kuitikia upendo wa Mungu. Kama ukisoma Warumi 2:6-7, utaona kwamba sisi sote tuna uamuzi. Mungu atawapa uzima wa milele wale -

> *"'ambao kwa saburi ya kuendelea kutenda mema **wanatafuta** utukufu na heshima na kutokufa. "*

Ikiwa tunatafuta utukufu yatupasa kuendelea kutenda mema, lakini kama hatutafuti; basi hakuta kuwa na tumaini la uzima baadaye.

Uzima wa milele na maisha yasio na mwisho

Utakuwa umegundua kwamba baadhi ya mafungu ya maneno tuliyo nukuu yanazungumzia kuhusu kutokufa (au uzima usio na mwisho), wakati baadhi yanatumia maneno "uzima wa milele". Uzima wa milele ni maisha ambayo yanaonyesha sifa za Mungu. Kama tukiishi maisha ambayo kweli ni ya utauwa, Mungu kwa neema yake atatuzawadia maisha yasio na mwisho.

KUWA NA UZIMA WA MILELE MAANA YAKE KUISH!
MILELE KATIKA HAKI NA UMOJA NA MUNGU

Utatolewa lini uzima wa milele?

Utatolewa na Yesu Kristo kwa waaminifu baada ya ufufuo toka wafu. Nabii Danieli a4iutazamia:

> *"Wengi wa hao walio lala katika mavumbi ya ardhi wata amka, baadhi kwa uzima wa milele. na wengine kwa aibu na kudharauliwa milele" (Danieli 12:2).*

Hii itakuwa wakati Yesu atakapo rudi na kuwaita walio lala katika ardhi. Wataitwa kwa sababu “wanalala" naye Bwana atawatoa kwenye kifungo cha kaburi ili wapate uhai.

> *"Maana saa inakuja, ambayo walio makaburini wote watasikia sauti yake. nao watatoka: walio fanya mema, kwa ufufuo wa uzima" (Yohana 5: 28, 29)*

Kama tuna imani, tutajaribu kuishi kwa kufuata maagizo ya Mungu.
Imani ya kweli itaonekana katika njia ya maisha ya mtu; itadhihirisha ufuasi wake kuwa ni wa kweli.

Sura za kusoma: Zaburi 32; Warumi 4; halafu soma tena Wagalatia 3; pia Tito 3:4 na 2:11-13
Jifunze kwa moyo: Warumi 5:1-2

UFUFUO KUTOKA WAFU

Soma:1 Wakorintho 15
Na 25.

Neno "ufufuo" maana yake ni kurudi kwenye uhai

Imekuwa ni tukio la ajabu sana katika historia ya ulimwengu, wakati Yesu alipotoka kwenye kaburi baada ya kuwa mfu siku tatu. Wanafunzi wake walipo muona, hawakuamini macho yao. Walidhani wameona roho, lakini Yesu aliwaambia:

"Tazameni mikono na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe: nishikeni na muone; maana roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo. Na baada ya kusema hayo, aliwaonyesha mikono yake na miguu yake. Na walipokuwa hawaja amini bado kwa furaha, nao walistaajabu, aliwaambia, mna chakula chochote hapa? Wakampa kipande cha samaki wa kuokwa na sega la asali Akachukua, naye akala mbele yao" (Luka 24:39-43).

Mwishowe, walithibitishiwa kwamba kweli alikuwa hai tena. Mungu alimleta kutoka wafu na alipwepa uzima wa milele. Tuna soma Yesu akisema:

> *"Tazameni, mimi ni hai milele" (Ufunuo 1:18).*

Yesu atawafufua walio mfuata

Yesu aliwafundisha wafuasi wake kwamba nao pia, watafufuliwa kutoka wafu. Angalia tena mstari tulio unukuu. Yesu aliendelea kusema:

> *"Mimi ni hai, na nilikuwa nimekufa; tazama, mimi ni hai milele hata milele, Ameni; nina funguo za kuzimu (au, kaburi) na mauti" (Ufunuo 1:18).*

Sasa, kama unazo funguo za mlango, ma maana kwamba una uwezo wa kufungua mlango huo. Yesu ana funguo za kaburi. Hii ni namna ya kusema kwamba ana uwezo wa kufungua makaburi, na kuwa weka huru ambao wamezikwa humo. Uwezo huu amepewa na Mungu. Soma Injili ya Yohana, sura ya 5, mstari wa 20-29. Angalia hasa mstari wa 21, ambao unasema:

> *"Maana kama Baba awafufuavyo wafu, na kuwahuisha; vivyo hivyo na Mwana awahuisha wale awatakao."*

Kuhuisha ni kuleta kwenye uhai; Mungu amempa Yesu uwezo wa kuwaleta wanaume na wanawake kwenye uhai tena.

Abrahamu aliahidiwa ufufuo

Tayari kama tulivyo jifunza katika Somo la 12, Mungu aliahidi ahadi kubwa kwa Abrahamu. Zilijumuisha:

> *"...nchi yote unayo iona, nitakupa wewe na uzao wako milele" (Mwanzo 13:15).*

Hata sasa tunajuwa kwamba Abrahamu alikufa bila ahadi hii kutimizwa. Abrahamu inabidi afufuliwe toka wafu ndipo Mungu anaweza kutimiza ahadi Yake. Bwana Yesu alitumia hoja hii sana katika kuthibitisha ufufuo wa wafu. Unaweza kusoma katika Mathayo 22:31-32.

Tena, Yesu aliwaambia Wayahudi wa siku zake kwamba watamuona Abrahamu, Isaka na Yakobo kwenye Ufalme wa Mungu, na wao wenyewe wakitupwa nje (Luka 13:28).

Hatuwezi kupata uzima wa milele

> "Mshahara wa dhambi ni mauti; bali **karama ya Mungu** ni uzima wa milele katika Yesu Kristo Bwana wetu" (Rumi 6:23).

Kama tulivyo ona, uzima wa milele ni zawadi ya Mungu, Hakuna hata mmoja wetu, ingawa ni mwema, anaye ustahili. Kama wenye dhambi, uzuri tunao weza kuufurahia na kuutegemea ni baadi ya faida ya uzima huu wa kuishi miaka 70 au 80 juu ya sayari hii basi.

UMBO LISILO NA MWISHO LA MUNGU (Zaburi 90:2)	UMBO LA MWANADAMU LINALO KUFA (Zaburi 90:10)
`Kabla milima haijaletwa au haija umbwa dunia na ulimwengu, na tangu milele hata milele, ndiwe Mungu."	"Siku za miaka yetu ni miaka sabini; na tukiwa na nguvu miaka themanini, bado muda wao ni shida na huzuni; maana muda unapita upesi na kutokomea mara."

Hivyo tunajuwa tutakwenda kaburini na kuoza, tusiwepo tena, **isipokuwa** tukiwa na tumaini la Biblia la uzima wa milele katika Yesu Kristo.

Watu wote walio julikana katika Biblia watu wakuu ambao walimwamini Mungu walikuwa na tumaini hili. Walitafuta kipindi kizuri kinacho kuja baadaye.

Angalia kile kilichosemwa kuhusu Abrahamu. Sara, Isaka. Yakobo, Daudi na wengi wengine (Waebrania 11:13).

"Wote hawa walikufa katika imani. **hawakuzipokea ahadi,** bali waliziona **kwa mbali,** na walisadikishwa nazo, na na walikiri kwamba walikuwa wageni na wasafiri juu a nchi."

Paulo na Yohana, kama mitume wengine, walitazama mbele kwenye uzima wa milele (ona Tito 1 :2; 1 Yohana 2:25).

"Katika tumaini !a uzima wa milele. ambalo Mungu hawezi kudanganya, ahadi alizo ziahidi kabla ya ulimwengu kuanza."

“Na hii ni ahadi aliyo tuahidi sisi yaani , uzima wa milele".

Muhutasari

1 . Kutakuwa na siku ya hukumu.
2. Utafuata ufufuo.
3. WOTE walio ijuwa kweli na kuielewa kweli ya Mungu wataletwa kwenye hukumu.
4. Watakao kubaliwa kwenye kiti cha hukumu wakati huo watapewa uzima wa milele.
5. Wale watakao kataliwa wataona uchungu wa moya, na wataangamizwa.

Sura za kusoma: 2 Wakorintho 5
Mstari wa kujifunza: 2 Wakorintho 5:10

> *"Maana yatupasa sote sisi kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo; ili kwamba kila mtu apate mambo aliyofanya katika mwili wake, kufuatana alivyo fanya, iwe mema au mabaya."*

UZIMA USIO NA MWISHU Na27

Soma: Yohana 3

Utakuwa tayari umefahamu katika kozi hii ya Biblia kwamba mtu wa kwanza Adamu aliumbwa na Mungu kwa kufanyiza mwili na kisha akampulizia pumzi ya uhai. Lakini Adamu na Eva walitenda dhambi na hivyo wakawa viumbe wanao kufa. Wanaume na wanawake wote mwishowe hufa, kwa sababu wote ni wenye dhambi, na adhabu kwa dhambi ni mauti (angali a Warumi 5:12). Sisi sote ni wenye kufa. Haidhaniwi kwamba wenye dhambi wataishi milele.

Mtu mmoja tu ndiye amefanywa kutokufa (kamwe asife tena), na huyo ni Yesu. Alizishinda nguvu za mauti kwa kuishi maisha yasio na dhambi. Hiyo ndio sababu Mungu alimfufua toka wafu {kwenye kaburi) na alimpa uzima usio na mwisho. Kwa kweli, Mungu Peke yake hafi; “Yeye ni tangu milele na milele". Ukimuweka Mungu kando, Yesu Kristo na malaika tu kwa sasa hawafi. Tafadhali soma 1 Timotheo 6:15-16.

Kitu cha ajabu kuhusu injili ni kwamba katika kuamini makusudi ya Mungu na kazi ya Yesu ya kuokuwa, imewezekana kwa **sisi** kuwa na tumaini la uzima usio na mwisho.

> *"(Neema ya Mungu) sasa imedhihirishwa kwa kufunuliwa mwokozi wetu Yesu Kristo aliye batili mauti, na ameleta uzima na kutokufa kwenye nuru katika injili ... " (2 Timotheo 1:10).*

Tumaini walilo shiriki watu wote waaminifu

Watu wa Mungu kwa nyakati zote wamekufa wakitazama mbele kwenye siku ambayo watafufuka wapate uzima tena. Paulo anatuambia baadhi ya watu hawa,

> "... walikufa katika imani, hawakuzipokea shadi bali waliziona kwa mbali" (Waebrania 11:13).

Zaidi anawataja watu hawa tena ambao

> *"...hawakupokea ahadi: kwa kuwa Mungu alituwekea sisi kitu bora ili kwamba pasipo sisi wasikamilishwe" (Waebrania 11:39-40).*

Tunaona kutoka mstari huu kwamba zawadi ya uzima wa milele watapewa waabudu wote wakweli wa Mungu kwa wakati mmoja.

Wakristo wa kwanzo nao pia walitazama kwenye muda huu mbele. Wakati mmojawao alipokufa, walimtaja kuwa amelala', kwa sababu kiasi kama watu wanapo amka baada ya usngizi, hivyo wafuasi wake wataamshwa kutoka kwenye usingizi wa mauti. Katika sura ya 15 1 Wakorintho, sura ambayo umekwisha soma, Paulo anasema zaidi ya wanafunzi 500 ambao walimuona Yesu baada ya kufufuka:

> *"Baadhi yao wamelala" (mstari wa 6).*

Tumaini hili la ufufuo na uzima wa milele walishiriki wafuasi wa kweli wa Yesu kutoka siku ile hadi leo.

Marafiki wa Yesu walielewa kwamba Yesu anaweza kuwafufua kutoka wafu

Yesu alikuwa na marafiki watatu, Lazaro na dada zake Martha na Mariamu, ambao walikuwa wanaishi Bethania, katika kijiji kidogo karibu na Yerusalemu. Siku moja, Lazaro aliugua. Dada zake walitumwa kumwita Yesu, lakini kwa muda ambao alifika, Lazaro alikuwa amekufa. Wakati Martha alipomuona Yesu, alimwambia:

"Bwana, kama ungalilkuwapo hapa, kaka yangu asingekufa."

Yesu alimwambia Martha:

"Ndugu yako atafufuka tena."

Sasa angalia jibu la Martha kwa makini. Alisema:

"Ninajuwa kwamba atafufuka tena kwenye utufuo wa siku ya mwisho."

Martha alijuwa kutakuwa na ufufuo wakati ujao. Yesu alimwambia:

"Mimi ni ufufuo na uzima."

Basi, ili kuwaonyesha wale walio kuwepo pale kwamba **ana uwezo wa kufufua wafu,** Yesu alimwita Lazaro kutoka kaburini. Naye Lazaro alitoka nje – hai!

Sio kama Yesu, Lazaro hakupewa uzima wa milele. Alikufa tena, lakini, kama Martha alivyo sema, atafufuka tena katika ufufuo wa siku ya mwisho. Ndivyo Yesu alivyowafundisha rafiki zake, walielewa nao walimwamini. Unaweza kusoma habari hii katika Yohana 11.

Kitu kilicho bora kuliko uzima wa leo

Kwa sisi sote maisha yana matatizo mengi. Wengi wetu tunajuwa kuumwa; tunapata wasiwasi kuhusu mambo mengi sana. Mauti yanaweza kuwa chukuwa tunao wapenda wakati wowote. Tunajuwa, pia, kwamba uzee inabidi uje kwa wakati wake, pamoja na uchungu wake wote na kuumwa. Je, tunapenda kuishi milele katika ulimwengu huu usio kamilika?

Uzima anao uahidi Yesu kwa wafuasi wake atakapo kuja tena ni kitu tofauti kutoka maisha yetu ya leo pamoja na mahangaiko yake yote. Katika maneno mazuri ya Ufunuo 7:16,17 tumeambiwa wale ambao watapewa uzima huo, kwamba:

"Kutakuwa na kilio na kusaga meno, wakati mkimuona Abrahamu na Isaka na Yakobo. na manabii wote, katika Ufalme wa Mungu, na ninyi wenyewe mtatupwa nje. " (Luka 13:28).

Mwishowe, wataangamizwa kabisa. Yesu alilinganisha hukumu na mavuno ambapo nafaka njema zilitengwa toka magugu yasio faa. Nafaka kwa uangalifu zinatunzwa, bali magugu yanateketezwa katika moto wa mkulima (Mathayo 13:36-43). Paulo alifundisha kitu kile kile kwa udhahiri sana:

"Bwana Yesu atafunuliwa toka mbinguni pamoja na malaika wa uwezo wake, katika mwali wa moto kuwalipa kisasi wale wasio mjuwa Mungu, na ambao hawakuitii injili ya Bwana wetu Yesu Kristo: ambao wataangamizwa kwa maangamizi ya milele mbele ya Bwana, na kutoka kwenye utukufu wa uwezo wake" (2 Wathesalonike 9:7-9)	WATU KUHUKUMIWA WENGINE WAKUBALIWA WENGINE WAKATALIWA PEWA UZIMA WA MILELE KUANGAMIZWA

Upendo au hofu?

Kuna baadhi ya mafungu ya maneno katika Biblia ambayo yanaonekana yanatuonya tusiwe mno majasiri kuhusu mahali petu kwenye hukumu; lakini Maandiko mengine yanaonekana yanatutia moyo kuwa na ushupavu tele. Kweli maneno hayaja achana. Tusiwe na ujasiri kwa sisi wenyewe - balituwe na ushupavu kabisa uwezo unao okowa wa Mungu. Maana, kama tunavyo soma Kwa Warumi 8:32:

"Ambaye hakumwachia Mwanawe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje pamoja naye kutupa mambo yote?"

Ingawa tunaweza kuanza kumuogopa Mungu, kidogo kidogo tutajifunza kumpenda na kumtumaini Yeye kabisa. Na hivyo Yohana anasema:

"Katika hili pendo lilikamilishwa kwetu, ili tuwe na ujasiri katika siku ya hukumu Hamna hofu katika pendo; bali pendo kamili huitupa nje hofu" (1 Yohana 4: 17-18).

Utaona kwamba wazo la kwenda mbinguni tunapo kufa halita faa katika kweli hizi za Biblia.

Furaha kwa wale ambao watakubaliwa

Wale watakao kubaliwa kwenye hukumu watapewa uzima wa milele. Miili yao kamwe haita ona tena uchungu au kuchoka au udhaifu wowote wa binadamu, na akili zao hazita jaribiwa tena kufikiri mawazo mabaya. Kitakuwa ni kipindi cha furaha kuu kwa waaminifu. Katika Biblia imesemwa ni kama siku kuu ya arusi, nasi tunasoma katika Ufunuo 19:9: "Heri ambao wamealikwa kwenye karamu ya Mwana Zondoo."

Wakati Yesu alipo kuwa na wanafunzi wake, akishiriki chakula chake cha mwisho pamoja nao duniani kabla ya kifo chake - tuna iita "karamu ya mwish" - ali waambia:

> *"Nawa wekea ninyi ufalme, kama Baba yangu alivyo niwekea; ili ninyi muweze kula na kunywa kwenye meza yangu katika ufalme wangu; na kuketi juu ya viti vya enzi kumi na mbili mkihukumu kabila kumi na mbili za lsraeli" (Luka 22:29-30).*

Wakati Ufalme utakapo kuja. mitume kumi na mbili watatawala juu ya Israeli. ambalo litakuwa wakati huo taifa la muhimu zaidi duniani. Kila mfuasi atakaye kubaliwa na Yesu atashiriki katika kazi ya kutawala ulimwengu. Hivyo tunasoma katika Ufunuo 5:9,10 kwamba watakatifu waaminifu waimba wimbo, wakisema:

> *"Ulichinjwa. na ulitukomboa sisi mpaka kwa Mungu kwa damu yako toka kila kabila, na lugha, na jamaa, na taifa: nawe umetufanya kwa Mungu wetu wafalme na makuhani: nasi tutamiliki juu ya nchi."*

Kutatokea nini kwa wale watkao kataliwa?

Tumeona kwamba wale watakao fika kwenye kiti cha hukumu cha Kristo watagawanywa katika makundi mawili. Baadhi Kristo atawakubali, na wengine atawakataa. Atawapa uzima wa milele kwa wale watakao kubaliwa. Lakini patatokea nini kwa wale atakao wakuta hawafai Adhabu yao itakuwa ni nini? Hatujui habari ya mambo moja moja, lakini baadhi ya mambo yapo dhahiri kabisa. Kwanza; wataona jinsi walivyo kuwa wapumbavu; watatambua namna baraka za ajabu walizo zitupilia mbali, na hii itawafanya waumie moyoni. Yesu alisema kwa watu kama hawa:

> *"Hawata ona njaa tena, wala hawata ona kiu tena; wala hawata pigwa na jua au joto lolote lile. Maana Mwana Kondoo aliye katikati ya kiti cha Enzi atawachunga, na kuwaongoza kwenye chemchem za maji yalio hai: na Mungu atayafuta machozi kutoka macho yao."*

Hawata kuwa na miili inayo oza tena, bali watashiriki roho - uzima wa Mungu Mwenyewe. Katika Marko 12:25 Yesu anasema:

> *"... wakati watakapo fufuka kutoka wafu, hawaowi, wala kuolewa; bali kuwa kama malaika walioko mbinguni."*

Wale ambao watapewa uzima wa milele na Yesu atakapo rudi watafurahia afya kamili na nguvu zisizo na kikono, watakuwa huru kutoka matatizo yote ya leo.

Ufufuo utatokea lini?

Karibu miaka 2,000 imepita tangu Yesu afufuliwe kutoka wafu. Atawafufua lini wale ambao "wamekufa katika imani"? Mtume Paulo anatujibia swali hili. Anasema katika 1 Wakorintho 15:22,23:

> *"Kwa maana kama katika Adamu wote hufa, kadhalika wote katika Kristo watahuishwa. Lakini kila mtu katika daraja lake mwenyewe: Kristo matunda ya kwanza; baadaye wale ambao ni wa-Kristo* ***atakapo kuja."***

Tayari tumeona kwamba Yesu Kristo anakuja tena ili kuuweka Ufalme wa Mungu na kutawala dunia yote. Atakapo kuja kufanya hivi, atawafufua wafu. Kisha wale ambao walikuwa waaminifu atawapa uzime wa milele, na watafurahia haki kubwa ya kumsaidia Yesu ya kutawala ulimwengu. Twasoma katika Ufunuo 5:9,10 maneno ya wimbo ambao wataimba siku hiyo:

"... ulichinjwa, nawe umemnunulia (umekomboa) Mungu kwa damu yako toka kila kabila, na lugha, na watu, na taifa; umetufanya kuwa wafalme na makuhani kwa Mungu wetu: nasi tutatawala juu ya nchi."

Wengine watakuwa hat wakati Yesu atakapo rudi tena

Vipi ambao wale watakuwa ha bado wakati Yesu atakapo rudi? Katika 1 Wathesalonike 4:14-17 Paulo anatuambia zaidi kidogo kuhusu hili. Anasema:

"Maana ikiwa twaamini kwamba Yesu alikufa na alifufuka tena, kadhalika pia waliolala katika Yesu Mungu atawaleta pamoja na ye. Maana hili twalisema kwenu kwa neno Ia Bwana, kwamba sisi tulio hai na kubaki hata ajapo Bwana hatuta watangulia walio lala. Kwa maana Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko wa sauti ya malaika mkuuu, pamoja na baragumu ya Mungu: na wafu katika Kristo watafufuka kwanza: kisha sisi tulio bakia hai tuta nyakuliwa pamoja nao mawinguni, kukutana na Bwana hewani: na hivyo tutakuwa na Bwana milele."	Tazama maneno *"kunyakuliwa pamoja mawinguni, kukutana na Bwana hewani".* Unaweza kudhani ni kwenda mbinguni. Lakini angalia tena. Paulo hasemi kukutana na Bwana mbinguni, bali kukutana naye hewani. Hivyo baada ya ufufuo wa wafu na kuwakusanya pamoja wanafunzi wale ambao wapo hai Bwana ajapo, wote ambao watakubaliwa watachukuliwa kwa muujiza ili kumsaidia Bwana Yesu katika kazi yake ya kutawala dunia. Kitu cha muhimu kwa wafuasi wote wa Yesu ni kwamba katika siku hiyo "watakuwa na Bwana milele"; hiyo ni kusema kwenye Ufalme wake duniani.

"Njoni ninyi mliobarikiwa na Baba, urithini ufalme ulioweka tayari kwa ajili yenu tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu" (Mathayo 25:34).

Yesu mwenyewe ndiye atakuwa mwamuzi (ona Yohana 5:28-3~), na atahukumu kwa hekima ambayo amepewa na Mungu. Tunasoma katika Isaya 11:

"Hatahukumu kwa kuyafuata ayaonayo kwa macho yake; wala hataonya kwa kuyafuata ayasikiayo kwa masikio yake: bali kwa haki atawahukumu masikini. naye atawaonya wanyenyekevu wa dunia kwa adili" (Isaya 11:3-4).

Watu wanaweza kuhukumu kwa kuona na kusikia; lakini Bwana Yesu ataijuwa mioyo ya watu, na hatafanya makosa katika maamuzi yake.

Nani watakuwa kwenye kiti cha hukumu

Wale ambao Bwana awahesabu wanahusika; ambao wamesikia neema ya Mungu ya kutoa '., uzima. na kujuwa wangejitoa, watakusanywa kwenye kiti cha hukumu cha Kristo

Lakini hawata kuwa hao tu. Kutakuwa na wanaume na wanawake walio ishi kabla ya Yesu, sambamba na wale walio ishi baadaye; wote wataitwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo kutoa hesabu kwa jinsi waliyofanya yaliyo husu ujumbe wa injili, "lulu yenye thamani kubwa". Wale ambao hawakuwa waaminifu watakuwa kwenye kiti cha hukumu pamoja na wale walio jaribu kuishi kwa kufuata mfano wa maisha makamilifu ya Yesu. Hebrania 10:26-27 inatuonya sisi:

"Maana kama tukifanya dhambi kwa kusudi baada ya kupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi, bali kuna kuitazamia hukumu halisi ya kutisha na ukali wa moto ulio tayari kuwala wapingao".

Yesu mwenyewe anatuambia: "Yeyote atakaye nikana mimi mbele za watu, nami pia nitamkana mbele ya Baba yangu aliye mbinguni" (Mathayo 10:33).

Wale ambao kamwe hawakumjuwa Mungu wa kweli, na plani yake ya ukombozi, hawata fufuliwa kwa ajili ya hukumu. Unaweza kukumbuka mistari hii katika Zaburi 49:19,20 ambayo inawasema watu kama hawa:

“Atakwenda kwenye kizazi cha baba zake; hawata ona kamwe nuru. Mtu ambaye yu katika heshima, na hana ufahamu, ni kama wanyama wanao potea."

"Sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo" (Warumi 94: 10) "Yatupasa sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo; ili kila mmoja apate mambo aliyo yafanya katika mwili wake; iwe alifanya mema au mabaya" (2 Wakorintho 5:10).

Kutakuwa na wakati wa kufanya hesabu

Yesu aliwahi mara moja kuwaambia wafuasi wake: "Ninyi mwaniita Mwalimu na 8wana: nanyi mwanena vema; maana ndivyo nilivyo" (Yohana 13: 13). Katika nyakati za Agano Jipya, kama mtu amemnunua mtumwa, anammiliki mtumwa yule kabisa. Mtumwa hawezi kujifurahisha mwenyewe; wakati ule mtumwa alikuwa na kazi moja katika maisha yake - ni kumpendeza bwana wake.

Sasa Yesu alitununua kwa damu yake, wakati alipo utoa uhai wake msalabani akiwa sadaka kwa dhambi, Basi Paulo anatuambia:

"Ninyi si mali yenu wenyewe. Maana milinunuliwa kwa thamani: kwa hiyo mtukuzeni Mungu katika viungo vyenu, na katika roho zenu, ambavyo vyote ni vya Mungu" (1 Wakorintho 6: 19,20).

Hii ina maana kuwa tunahusika kwa Bwana Yesu kwa njia tunayo ishi maisha yetu. Wakati ajapo tena atawazawadia waaminifu, na atawaadhibu wale ambao wamedharau njia zake

Kweli katika mfano

Kuwafundisha wafuasi wake shughuli zao kwake, Yesu aliwaambia mfano ambao utaupata katika Mathayo 25:14-30. Sasa soma mwenyewe. Angalia mstari 21 , ambao unasimulia ujira wa watumishi waaminifu: “... Ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mambo mengi: ingia katika furaha ya Bwana wako."

Mtu ambaye hakutii hawezi kutegemea ujira kama huu. Adhabu yake ni kali. 4na mstari wa 30: "Mtupeni nje mtumwa asiye na faida kwenye giza la nje: ndiko kutakuwa na kilio na kusaga meno."

Muhukumu wa haki

Yesu atakapo kuja tena, atawafufua wafu, na kuwakusanya pamoja wafuasi wake ambao watakuwa hai wakati huo. Kutakuwa na wakati wa hukumu. Baada ya hukumu; wale ambao watakubaliwa watapewa uzima wa milele, naye Yesu atawaambia:

Huwezi kuwa na njia mbili

Watu wengi - mara nyingi watu ambao huwa wana amini uzima baada ya mauti - wanaume na wanawake wanaamini kwamba wanakwenda mbinguni wakifa. Mwili unao kufa unalazwa kaburini. Lakini, wanasema, mtu ana "roho" au "nafsi" ambayo inaendelea kuwa hai wakati mwili ukiwa umekufa. Wakati mtu anapokufa, roho hii inakwenda mbinguni kuwa na Mungu.

Biblia, kwa upande mwingine, inasema waziwazi kwamba Yesu atarudi tena duniani na kufufua wafu.

Sasa ***mawazo mawili hayawezi kuwa sawa.***

Kuisema nafsi ambayo imekuwa na Mungu mbinguni inarudi tena kuungana na mwili na kuletwa kwenye hukumu ni upuuzi. Biblia haisemi chochote kuhusu mtu yeyote kuwa ana kwenda mbinguni. **Inasema** kwamba wanafunzi watalala kaburini, wakiwa hawana fahamu mpaka Bwana awafufue kutoka wafu atakapo kuja.

Kristo ana rudi lini (wakati Kristo ajapo)

Wote ambao wameisikia Injili wataletwa mbele ya Kristo Bwana Yesu. Wafu watafufuliwa na walio hai watakusanywa pamoja. Kabla ya kuwapa baadhi yao uzima wa milele, pale inabidi kuwe na hukumu - lakini utasikia zaidi kuhusu hiyo katika somo litakalo fuata.

Soma tena 1 Wakorintho 15:51-58. Hapa mtume anazungumzia kipindi wakati Wakristo waaminifu watapewa zawadi hiyo kubwa ya uzima wa milele - au, kama anavyo iita hapa, kutokufa. Kama tunavyo tazama mbele kwenye kipindi hicho, mtume Paulo anatuambia *"tuimarike, tusitikisike, siku zote tudumu katika kazi ya Bwana"*

Muhutasari

1. Mungu amempa Yesu uwezo wa wakufufua wafu.
2. Atafanya hivi wakati atakapo rudi duniani kuusimamisha Ufalme wake.
3. Wakati uleule, atawakusanya wale "walio katika Kristo" ambao watakuwa hai wakati atakapo rudi.
4. Kwa wale ambao watakuwa waaminifu, atawapa uzima wa milele, nao wata ishi na kutawala pamoja nave duniani.

Sura za kusoma:

I Wathesalonike 4; Waebrania 11; Yohana 11; Mathayo 22:23-33

Mistari ya kujifunza: Yohana 5:28,29

> *"Msistaajabu: kwa maana saa inakuja, ambayo wote walio makaburini watasikia sauti yake, nao watatoka; walio fanya mema, kwa ufufuo we uzima; na walio fanya mabaya, kwa ufufuo wa hukumu."*

HUKUMU
Na.26

Soma: Mathayo 25

Yapasa Mungu kumtii

Wakati Mfalme Daudi alipowekwa kweye kiti chake cha enzi, aliazimu kuleta Sanduka la Agano na Mungu kutoka Kirjath-jearim, Yerusalemu. Mkokoteni mpya ulitengenewa wa kuvutwa na ng'ombe. Wakati yote yalipo kuwa tayari, makuhani wa Mungu walitembea ubavuni mwa saduku kwa kadri lilivyo endelea kwenye njia yake. Mahali fulani ng'ombe walijikwaa, na mtu mmoja aliye itwa Uza aliweka mikono

yake ili kulishika sanduku lisianguke. Ndipo tunaambiwa, kitu cha kuogofya kilitokea:

> *"Mungu alimpiga huko kwa kosa lake; na palepale akafa" (2 Samweli 6:7).*

Kwa nini adhabu ilikuwa kali mno, wakati yote ambayo Uza aliyafanya ilikuwa ni kuzuia sanduku la Mungu lisianguke? Mungu alisema waziwazi kabisa katika kitabu cha Hesabu kwamba sanduku Lake yapasa **lichukuliwe na makuhani juu ya mabega yao.** Hivyo pengine Uza hakujua amri ya Mungu, au hakuchagua kuitii. Katika jambo mojawapo, alikuwa na hatia mbele za Mungu.

Sababu hii inatuonyesha sisi kwamba Mungu ni mtakatifu na ni mkuu, na kwa haki anataka utii kutoka wale ambao wanamtumikia Yeye

Watu wanao dharau upendo wa Mungu

Yesu aliwahi kusimulia mara moja mfano ulio husu mfalme aliye andaa siku kuu ya arusi kwa ajili ya mwanawe. Siku kuu ilipo kuwa tayari aliwatuma watumishi wake kuwaita wageni; lakini wageni wale walikataa kwenda! Walipenda kushirikiana na mambo yao ya kila siku kuliko kutii mwaliko wa mfalme kwenda kwenye arusi. Sio ajabu mfalme alikasi rika, naye aliwatuma watumishi wake kuwaangamiza walio dharau mwaliko wake (Mathayo 22:1-14).

Mungu ni Mfalme mkuu. Kama kwa neema amemwalika mwanaume au mwanamke kuja kushiriki katika furaha ya ufalme wake duniani, na mtu huyo kwa makusudi akasema, "Sihitaji anachonipa Mungu, na sitamtii" - basi utakuja wakati wa hukumu, na mtu huyo atahukumiwa. Kama tunavyo soma kwa Wagalatia 6:7: "Mungu hazihakiwi: kwa maana chochote mtu apandacho, ndicho atakacho vuna. "

Ufufuo na hukumu

Biblia inatufundisha kwamba kutakuwa na siku ya hukumu baada ya ufufuo. Mungu ni pendo; bali pia ni mwenye haki na ni mnyoofu. Kama inavyo semwa katika Kutoka 34:7, "Hasha (Mungu) hataondoa hatia". Hataweza kutoa uzima wa milele kwa wanaume na wanawake walio lidharau pendo lake, na ambao - wanajuwa kwamba Yesu alikufa kwa ajili yao hawakufanya bidii kumtumikia na kumtii. Hivyo Paulo anatuambia:

Kama unataka kujifunza zaidi njia ya Mkristo wa kweli anavyopaswa kuishi, basi ni lazima ujifunze Biblia. Ili kukusaidia; Kanise la Christadelphian Bible Mission limechapisha kijitabu kuhusu mafunzo ya Biblia kaitka somo hili muhimu.

Lina itwa Kuishi katika Ukweli. Unaweza kupata nakala kutoka Kanisa la Christadelphian, au kutoka anuani iliyoandikwa katika kijitabu hiki.

CBM Publishing
32 Blenheim Road, Far Cotton
Northampton, England. NN4 8NW

ISBN 1 902059 09 -3
Registered Charity Number: 248979 / 1020558
Company Number: 2796412

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIAN 24-27
Correspondence Course Lessons 24-27